**SALAMU ZA KAIMU MKUU WA MKOA WA DODOMA, MHE. DR. REHEMA J. NCHIMBI WAKATI WA MAPOKEZI YA MWENGE WA UHURU MPAKANI MWA MIKOA YA MOROGORO NA DODOMA TAREHE 19 JUNI, 2017**

Mhe. Dkt. Kebwe Steven Kebwe
**Mkuu wa Mkoa wa Morogoro,**

Ndugu Amour Hamad Amour
**Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2017,**

**Spika wa Bunge Mheshimiwa Job Ndugai,**

**Ndugu Makatibu Tawala wa Mikoa ya Dodoma na Morogoro,**

Wahe. Viongozi wa Chama cha Mapinduzi wa Mikoa ya
**Dodoma na Morogoro,**

**Wahe. Wakuu wa Wilaya za Mikoa ya Dodoma na Morogoro,**

Ndugu Wajumbe wa Kamati za Ulinzi na Usalama Mikoa ya
**Dodoma na Morogoro,**

**Waheshimiwa Wabunge wa Mikoa ya Dodoma na Morogoro,**

**Ndugu Wakimbiza Mwenge Kitaifa,**

**Wahe. Viongozi wa Vyama mbalimbali vya Siasa,**

Wahe. Mameya na Wenyeviti wa Halmashauri za Wilaya za Mikoa ya
**Dodoma na Morogoro**

**Ndugu Viongozi wa Madhehebu mbalimbali ya Dini,**

**Wakuu wa Idara na Taasisi wa Mikoa ya Dodoma na Morogoro,**

**Ndugu Wanahabari,**

Wananchi mliohudhuria katika tamasha hili fupi la mapokezi ya Mwenge wa Uhuru hapa Mkoani Dodoma katika Kijiji cha Pandambili Kongwa.

**Asalam Aleikum........!!!**

**Bwana Yesu Asifiwe......!!!**



Scanned by CamScanner

**Awali ya yote** namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia Afya njema na kutukutanisha hapa leo katika tukio hili muhimu la mapokezi ya Mwenge wa Uhuru mwaka 2017. Naomba kutumia fursa hii kuwatambulisha Viongozi wa Mkoa wa Dodoma ambao tumefuatana nao katika msafara huu wa leo ambao ni: **(Orodha ya Wajumbe wa Msafara)**

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa**,

Napenda nitumie fursa hii kwa niaba ya Uongozi wa Serikali ya Mkoa na wananchi wote wa Mkoa wa Dodoma Makao Makuu ya Nchi yetu, kukukaribisha sana wewe binafsi na Wakimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa na Itifaki nzima ya Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2017 kwenye Mkoa wa Dodoma.

Aidha, Napenda kukupongeza wewe binafsi na Wakimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa mwaka 2017 kwa kazi kubwa na iliyotukuka ambayo mmeifanya kwenye mikoa mbalimbali mliyopita na hatimaye leo mnaingia Dodoma Makao Makuu ya Nchi yetu. Sisi Mkoa wa Dodoma tunaahidi kuwapa ushirikiano mkubwa, tunaahidi kuwaangalia afya zenu kwa umakini mkubwa, na tumehakikisha tunawawekea mazingira wezeshi kwenu kuwafikishia wananchi wa Dodoma Ujumbe wa Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2017 hadi pale tutakapowakabidhi kwa wenzetu wa Mkoa wa Singida.



Scanned by CamScanner

**PONGEZI KWA MHESHIMIWA RAIS DKT. JOHN POMBE MAGUFULI**

**Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Morogoro na Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,**

Kabla sijazungumzia mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2017 kwenye Mkoa wa Dodoma, Nitumie fursa hii adhimu kwa niaba ya Uongozi wa Serikali ya Mkoa wa Dodoma na Wananchi wote wa Mkoa wa Dodoma, kumpongeza sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na Serikali yake ya Awamu ya Tano kwa kuonesha Uzalendo Mkubwa na Jitihada zake za kusimamia Rasilimali za Nchi yetu na kudhibiti wizi na ubadhirifu wa Rasilimali za Taifa, hususani kwenye upande wa Madini. Sisi Uongozi wa Mkoa na Wananchi wote wa Dodoma kwa ujumla tunamuunga Mkono Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli, Tunamuombea sana kwa Mwenyezi Mungu na pia tunamtakia kila la kheri katika kuliongoza Taifa letu Tanzania, na kila mmoja wetu atasimama vema katika nafasi yake, kwa Utiifu, Uaminifu na Uadilifu.

**Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Morogoro na Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa**, mwaka huu, Mwenge wa Uhuru utapita kwenye Wilaya saba (7) za Mkoa wa Dodoma ambazo ni Kongwa, Mpwapwa, Chamwino, Dodoma Mjini, Bahi, Chemba na Kondoa kwa umbali wa **Km. 1375** na kupitia jumla ya miradi **55** yenye thamani ya shilingi **20,045,637,896.** Kati ya miradi hiyo miradi **9** itafunguliwa, miradi **17** itazinduliwa na miradi **22** itawekwa mawe ya msingi. Aidha, miradi **6** itatembelewa na mradi **1** utakabidhiwa. Utekelezaji wa Miradi yote hii ambayo ni sehemu tu ya shughuli mbalimbali za maendeleo



Scanned by CamScanner

zinazotekelezwa Mkoani Dodoma, umefanikiwa kutokana na ushirikiano mkubwa kati ya Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Wananchi na Wadau mbalimbali wa Maendeleo.

Mchanganuo wa gharama za miradi hii ni kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| • Serikali Kuu | Tsh. | 6,807,356,143 |
| • Mamlaka za Serikali za Mitaa | Tsh. | 1,339,988,643 |
| • Wananchi | Tsh. | 2,156,027,530 |
| • Wadau wa Maendeleo | Tsh. | 9,742,265,580 |
| **JUMLA** | **Tsh.** | **20,045,637,896** |

## UJUMBE WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU MWAKA 2017

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,**

Wananchi wa Mkoa wa Dodoma wana shauku kubwa ya kupokea Ujumbe wa Mwenge wa Uhuru mwaka 2017 ambao utatolewa katika maeneo mbalimbali ya Wilaya za Mkoa wa Dodoma ambao ni **"Shiriki Kukuza Uchumi wa Viwanda kwa Maendeleo ya Nchi yetu"** tukitambua kabisa kuwa vipaumbele na mikakati ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kuifanya Nchi yetu kuwa na uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025 kupitia kukuza sekta ya viwanda kwa kufufua vilivyosimama uzalishaji na kuanzisha vipya vidogo vidogo na vikubwa. Uongozi wa mkoa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali tumeweka mikakati ya kuendelea kuhamasisha na kuvutia wadau mbalimbali wawekeze kwenye viwanda vinavyotumia malighafi inayozalishwa na wakulima wetu hapa Dodoma kama viwanda vya Mvinyo, Alizeti na nafaka zingine na Viwanda vya nyama na bidhaa za Ngozi ili kukuza soko la mazao ya wakulima na Wafugaji wetu. Aidha, Mkoa upo kwenye mkakati wa kuanzisha kituo kimoja cha



Scanned by CamScanner

kutolea huduma za kiuwekezaji yaani "One Stop Center" lengo likiwa kuboresha mazingira ya kiuwekezaji na utatuzi wa changamoto zinazowakabili wawekezaji waliopo Mkoa wa Dodoma.

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,**
Wanadodoma tunatambua pamoja na ujumbe huo zipo jumbe nyingine ambazo zimelenga mapambano Dhidi ya Dawa za kulevya chini ya kaulimbiu "tuwajali na tuwasikilize watoto na vijana", Mapambano dhidi ya rushwa chini ya Kaulimbiu "tuungane kwa pamoja dhidi ya Rushwa kwa maendeleo, amani na usalama wa Taifa letu". Vilevile, Mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI chini ya kaulimbiu "Tanzania bila maambukizi mapya, unyanyapaa na vifo vitokanavyo na UKIMWI inawezekana ifikapo mwaka 2030 na mwisho kabisa ni mapambano dhidi ya ugonjwa wa Malaria chini ya Kaulimbiu "Shiriki kutokomeza Malaria kabisa kwa manufaa ya Jamii"
Uongozi wa Mkoa unatambua kuwa Rushwa ni adui wa haki na maendeleo, Halikadhalika Madawa ya kulevya yanaathiri nguvu kazi ya Taifa letu na hivyo kurudisha nyuma maendeleo ya nchi yetu na hata kuigharimu Serikali fedha nyingi kwa malengo ya kuzuia na hata kutibu waathirika wa madawa. hivyo, Serikali ya Mkoa kwa kushirikiana na Mamlaka zinazohusika na Wadau mbalimbali tunaendelea na mkakati wa kutoa elimu na kuhamasisha kupiga vita rushwa na madawa ya kulevya maeneo mbalimbali kama mashuleni na maeneo ya huduma kwa jamii. Aidha, kupitia vyombo vyetu vya ulinzi na usalama tumeendelea kuchukua hatua kwa kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria wale wote wanaojihusisha na dawa za kulevya. Hivyo, naendelea kutoa wito kwa wananchi wa Dodoma kuendelea kutoa ushirikiano mkubwa kwa serikali kwenye vita hivi dhidi ya Rushwa na madawa ya kulevya.



Scanned by CamScanner

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru,** kasi ya kusambaa kwa VVU/UKIMWI, Unyanyapaa na Vifo vitokanavyo na UKIMWI inahatarisha na kudhoofisha jitihada za Taifa letu na Wananchi wake kujiletea maendeleo na kukuza uchumi kwa kuendelea kupoteza nguvu kazi ya Taifa hili, Hali kadhalika, Malaria nayo Bado imeendelea kuwa tatizo na kuigharimu jamii na Serikali fedha kwa lengo la kuendelea kuendesha kampeni za kuzuia na kutibu ugonjwa huu, hususani kwa watoto na akina mama wajawazito.

Takwimu zinaonesha kwa sasa kiwango cha maambukizi ya VVU kwenye Mkoa wa Dodoma ni asilimia 2.6% wakati kile cha kitaifa ni 5.7%, Mkoa kwa kushirikiana na wadau tunaendelea kuhimiza mabadiliko ya tabia, kuhimiza watu kupima na kujua hali zao za kiafya na kuhimiza kuacha ngono zembe na matumzii ya mipira ya kondomu, lakini pia kuendelea kutoa huduma kwenye kliniki za tiba, ushauri nasaha na kutoa dawa za kupunguza makali ya UKIMWI kwa waathirika

Kwa upande wa mapambano dhidi ya Malaria, Takwimu zinaonesha kuwa kiwango cha maambukizi ya Malaria kwa watoto chini ya miaka mitano (5) kitaifa ni asilimia 14% wakati kimkoa ni asilimia 1% (Malaria Indicator Survey 2015/16) Katika kuhakikisha tunaondoa kabisa tatizo la Malaria, Mkoa wa Dodoma umekuwa ukitilia mkazo mkubwa katika kuhakikisha kuwa yapo matumizi sahihi ya vyandarua vyenye dawa ya kuzuia mbu waenezao malaria, kuhimiza tabia ya wananchi kuhakikisha wanatibiwa mapema mara wanapoona dalili za malaria au homa, lakini pia wananchi wanahimizwa kuhakikisha kuwa wanaweka mazingira yao katika hali ya usafi ili kuzuia mbu kuzaliana na hivyo kusababisha kuwepo kwa mbu



Scanned by CamScanner

wanaoeneza malaria, hii ikiwa ni pamoja na kutekeleza Agizo la Makamu wa Rais Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan la kufanya usafi wa Mazingira kila jumamosi ya mwisho ya kila Mwezi.

**HITIMISHO**

**Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro na Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,**

kwetu Dodoma, Mwenge wa Uhuru ni Darasa la kuibua, kujenga, kuimarisha, kukosoa, kurekebisha, kuboresha usahihi wa uadilifu na ufahamu wetu ili kusimama vema katika misingi ya uzalendo, uadilifu, utumishi na hofu ya Mungu kwa mafanikio endelevu ya jamii na Taifa la Tanzania.

Mwisho kabisa, nirudie tena kwa niaba ya Uongozi wa Serikali ya Mkoa na wananchi wote wa Mkoa wa Dodoma Makao Makuu ya Nchi yetu, kukushukuru Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro na Wananchi kwa kuutunza Mwenge na Itifaki yake kwa muda wote Mwenge ulipokuwa Mkoa wa Morogoro. Aidha, kukukaribisha sana wewe binafsi Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2017 na Wakimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa na Itifaki nzima ya Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2017 kwenye Mkoa wa Dodoma. Karibuni Sana, Mungu awatunze, Mungu awabariki sana, Mungu ibariki Dodoma, Mungu ibariki Tanzania.

**MWENGE WA UHURU OYEE! DODOMA OYEE!**

**Dkt. Rehema Nchimbi**
**KAIMU MKUU WA MKOA**
**DODOMA**
Juni 19, 2017



Scanned by CamScanner